# MARIA NI MAMA

**Conrad Mghanga**




*All Rights Reserved. St.Francis Xavier Choir Msa / 2014*

# MARIA NI MAMA






**MARIA NI MAMA**

*Ni Maria mama, ni Maria mwombezi, ni Maria mama mzazi wa Mungu x2 (mama) Maria mama wa Mungu Maria, mzazi wa Mwokozi ni Maria, alishuhudia mateso yamwanawe,hakika anastahili kuwa mama .*

**1. Men:Ulimzaa Yesu Mwokozi mama, ukamleta hapa duniani mama,**
**Ladies: (Ndipo sasa tunasema wewe ni mama, ndipo sasa twangaza, wewe ni mama) x2 aeh**
**2. Men:Ukombozi ulitua ulimwenguni, ulipokubali ombi la malaika**
**Ladies: (Daima wewe ni mama, ni mama yetu, tangu sasa na milele, wewe ni mama) x2 aeh**
**3. Men:Malezi yako mama ni ya kipekee, yalidhihirika kwa huyo mtoto Yesu**
**Ladies: (Hakika pokea sifa, wewe ni mama, kwa kazi uloifanya pongezi mama) x2 aeh**
**4. Men:Ulivumilia mateso ya mwanao, ukayaona pia na mauti yake**
**Ladies: (Kwa kweli tunatambua, uzazi wako, sisi wana wako hapa, ulimwenguni) x2 aeh**
**5. Men: Mungu Mwenyezi kweli alikutambua, tangia mwanzo mpaka mwisho wa dahari**
**Ladies: (Kwani maisha yako, yalipendeza, mwishowe ukapalizwa, mbinguni kwa baba)x2 aeh**